

# Dalili hizi zinatishia uzalishaji korosho

**Kuna haja kubwa ya kupata miche mipya kwa kuwa iliyopo shambani imezeeka na haizalishi korosho za kutosha.**

Polycarp Machira, Mwananchi

Pamoja na ukweli kwamba mahitaji ya korosho duniani yataendelea kuongezeka, uzalishaji nchini Tanzania utaendelea kushuka kutokana sababu mbalimbali. Nyingi ya sababu hizo ni mazingira mabovu ya biashara.

Utafiti uliofanyika hivi karibuni unaonyesha kwamba dunia inahitaji sana korosho kutoka katika Bara la Afrika kukiwa na ongezeko la asilimia nane kila mwaka.

Takwimu zilizotolewa na Bodi ya Korosho nchini (CBT) zinaonyesha uzalishaji wa korosho umeongezeka kwa tani 120,000 kwa mwaka 2010/2011 kutoka tani 75,000 ambazo zilipatikana msimu wa mwaka 2009/2010.

Utafiti unaonyesha kwamba ukuaji wa kiwango cha uzalishaji hauwezi kuendelea kwa muda mrefu ujao kutokana na changamoto mbalimbali ambazo kwa sasa zinastahili kuangaliwa kwa makini.

Upo ukweli kwamba mingi ya mikorosho imezeeka kutokana na umri mkubwa wa miti hiyo.

**Miti ya korosho imezeeka**

Utafiti uliofanywa na Jukwaa la Kilimo la Taasisi zisizo za kiserikali (ANSAF) unaonyesha kwamba miti imezeeka na kutishia uzalishaji wa korosho itakapofika mwaka 2020. Utafiti huo pia umebainisha kwamba zaidi ya miti milioni 15 iliyopandwa kabla ya mwaka 1985 imefikia ukomo wa kuzalisha korosho.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Audax Rukonge, anasema utafiti uliofanyika unaonyesha kwamba kunahitajika Dola 110 milioni za Marekani kununua miche ya mikorosho na kuipeleka kwa wakulima ili waongeze mavuno ya korosho.

Tanzania inakadiriwa kuwa na kati ya miti milioni 40-50 ya mikorosho ambayo mingi yake imepandwa kati ya miaka 1950 na 1960 huku upandaji wa miti mipya ukizidi kuporomoka kuanzia miaka ya 1970. Utafiti umebaini kwamba wakulima walianza kupanda tena miti ya mikorosho miaka ya 1990.

Pamoja na kuwapo kwa mikorosho mipya bado ile yenye uwezo wa kuzaa ni kati ya milioni 20 hadi 25.

"Kuna haja kubwa ya kupata miche mipya, hii iliyopo ni mizee na haizalishi korosho za kutosha," anasema Rukonge.

Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho nchini, Mfaume Juma pamoja na kukiri kwamba suala la miti iliyozeeka ni tatizo kubwa pia ameweka wazi kuwa wakulima wana nafasi ya kupata miche mipya ili kukabiliana na tatizo hilo.

Anasema changamoto ya miti iliyozeeka inatofautiana kati ya mkoa na mkoa na eneo na eneo na kwamba wapo baadhi ya wakulima ambao wamepata miti mipya ili kuondokana na ile iliyozeeka.

Mikoa inayojulikana kwa kilimo cha korosho ni pamoja na Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma na Dar es Salaam. Hata hivyo uzalishaji wa korosho Mkoa wa Pwani umeendelea kushuka kutokana na wakulima kupoteza hamu ya kulima korosho.

"Wakulima wa Mkoa wa Pwani wanatakiwa kuamshwa ili kuongeza uzalishaji wa korosho. Haifai kuacha zao la korosho kuporomoka kama ilivyotokea kwa zao la nazi," anabainisha Juma.

Mtafiti kutoka Chuo cha Utafiti Naliendele, Dk Peter Masawe anakubaliana na ukweli kwamba ipo haja ya kupanda miti mipya ya korosho ili kubadili iliyozeeka ingawa ipo mikorosho mizee ambayo bado inazalisha korosho.

Katika msimu wa 2012/2013, wakulima katika Mkoa wa Pwani walizalisha tani 9,000 kati ya tani 120,000 zilizopatikana.

Pamoja na ukweli kwamba kuna miti mingi iliyozeeka, baadhi ya mikoa hivi sasa imeageukia kilimo kingine cha mazao yanayomea kwa haraka kwa kutumia pembejeo zenye gharama kidogo. Wakulima wamekuwa wakifadhaishwa na utaratibu wa kupata pembejeo kutoka katika kampuni za pembejeo ambazo zimeshinda zabuni ya serikali ya kupeleka pembejeo kwa wakulima. Pembejeo hizo ni zile ambazo Serikali inatoa ruzuku.

Tatizo kubwa linalozungumzwa wazi na wakulima takriban wote ni kupokea pembejeo pungufu kutoka kwa wafanyabiashara husika. Lakini mwaka jana mfumo ulibadilishwa kutokana na matatizo yaliyobainika msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012.

Mkazi wa Liwale, Mohamed Mpoto anasema wakulima wengi katika eneo lake wameanza kulima ufuta kwa kuwa zao hilo halina gharama kubwa kama ilivyo kwa zao la korosho ambalo pia soko lake ni la kubabaisha.

Pembejeo ya kudhibiti ukungu (sulphur dust) inauzwa Sh20,000kwa kilo mpaka Sh35,000. Bei yake bila ruzuku kwa tani ni Dola 1,265 za Marekani.

Bei ya kiuatilifu (sulphur) ni Dola 680 za Marekani kwa tani. Bei ya kiuatilifu aina hiyo ambayo inazalishwa Marekani, tani moja inauzwa Dola 200 za Marekani na mpaka kufika nchini ni Dola 680 za Marekani kwa tani.


"Ni dhahiri kwamba kuna gharama kubwa za kuleta na kusambaza pembejeo hizo nchini. Pamoja na hayo bei ya kiuatilifu inakuwa juu hata baada ya kuingizwa kwenye ruzuku," anabainisha.

Pamoja na ukweli huo pia kuna ucheleweshaji wa pembejeo. Mathalani wakulima wanatakiwa kupulizia miti yao Aprili, lakini mara zote wanapata viuatilifu Julai. Wataalamu wanasema kuna upotevu wa mazao kwa asilimia 80 hadi 100 kama miti hiyo haitapuliziwa dawa kwa muda husika.

Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Christopher Chiza anasema wanatambua matatizo hayo katika zao la korosho na kwamba wanazifanyia kazi ili kuyatatua, lakini hakuweza kueleza kinagaubaga ni hatua zipi zinachukuliwa, japo anasema katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 watu watashuhudia mabadiliko mengi yenye lengo la kuimarisha zao hilo.

**Tujadiliane kupitia ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kisha ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni bure, hautozwi.**

**NINI KIFA NYIKE?**



**-Kuongeza ubora wa zao la korosho.**

**-Kupunguza kodi kubwa katika zao la korosho zinazosafirishwa nje.**

**-Kupunguza gharama za pembejeo zinazoingizwa kutoka nje.**

**-Kupanda mikorosho mipya yenye uwezo wa kukabiliana na maradhi na inayozalisha korosho nyingi.**

Baadhi ya magunia yenye korosho yakiwa nje katika ghala la kutunza zao hilo mkoani Pwani. **Picha na Maktaba.**

**TAARIFA ZAIDI**

**"Zao la korosho linahitaji huduma nyingi zenye gharama, lakini faida yake ni ndogo. Hatuwezi kuhimili changamoto zinazokabili zao hilo kwa kuwa Mungu ametupatia raslimali nyingine, acha tufaidike nayo," anasema mkulima wa Mtwara, Abdallah Juma.**

**Ugunduzi wa mafuta na gesi katika mikoa ya Mtwara na Lindi kumeelezwa pia kuwapo kwa tishio katika zao la korosho.**

**Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) limesema kuna kampuni nane za Uingereza, Brazil na Norway yanafanya utafiti wa kutafuta mafuta na gesi baharini.**

**Kutokana na kuwapo kwa kazi hizo wakulima wameanza kuacha kilimo cha Korosho na kwenda kutafuta kazi katika kampuni hizo.**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI